TANGAZO LA SERIKALI NA. 211 la tarehe 22/3/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 8(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MJI MAFINGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji Mafinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"bidhaa" maana yake ni vitu mbalimbali vinavyoweza kuuzwa na kununuliwa katika duka, soko au eneo la mnada;

"burudani" maana yake ni sherehe, michezo, muziki na au shughuli yeyote ile ya kijamii inayohusisha kusanyiko la watu, isipokuwa kusanyiko la msiba:

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au wanyama wanaotumika

kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Mafinga;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kodi ya pango" maana yake ni kiasi cha fedha ambacho kitatozwa na Halmashauri ikiwa ni malipo ya pango la kukodi chumba cha ofisi, kibanda, meza au kizimba katika maeneo ya Halmashauri kwa kipindi maalum;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi ikiwa ni pamoja na maeneo ya taasisi ya umma au watu binafsi yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnunuzi wa mazao" maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni, kiwanda au shirika linalonunua mazao kwa ajili ya biashara au matumizi mengineyo katika eneo la Halmashauri;

"muuzaji" maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni, kiwanda au shirika linalouza au kusafirisha mazao kutoka kata moja kwenda kata nyingine au nje ya eneo la Halmashauri yenye uzito wa zaidi ya tani moja;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa;

"stendi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Halmashauri kutekeleza majukumu chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali au leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu mwenye wajibu wa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atapaswa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa ukusanyaji wa ada au ushuru

6.-(1) Ada au ushuru utakusanywa kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano kati ya Halmashauri na mlipaji.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ada au ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu mwenye wajibu wa kulipa atashindwa kulipa ada au ushuru ndani ya muda uliobainishwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Endapo mdaiwa atashindwa kulipa deni la ada au tozo ndani ya siku thelathini tangu kukamatwa kwa mali kwa mujibu wa aya ndogo ya (2), Halmashauri, baada ya kupata idhini ya mahakama, inaweza kuziuza mali hizo kwa njia ya mnada.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri, baada ya kupata idhini ya mahakama, inaweza kuuza mali hizo kabla hazijaharibika.

(5) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa notisi ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

8.-(1) Halmashauri inaweza kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kuwa wakala wa kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria

Ndogo hii;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

(3) Wakala atahakikisha malipo ya ushuru yanafanyika kwa njia ya kielektroniki na risiti zinatolewa kwa kila muamala.

Maeneo ya machinjio

9. Mtu anayekusudia kuchinja mnyama kwa ajili ya biashara, atachinja mnyama wake katika machinjio yatakayobainishwa na Halmashauri.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

11.-Wakala ambaye-

(a) atakusanya ushuru bila kibali cha maandishi cha Halmashauri;

(b) atakusanya ushuru kwa kiwango tofauti na kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha kiwango pungufu cha ushuru uliokusanywa;

(d) atakusanya ushuru kwa mbinu tofauti na zilizoelekezwa na Halmashauri,

anatenda kosa.

(2) Mtu ambaye-

(a) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kikundi cha watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;
(e) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; au
(f) atatumia chombo chochote kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

12. Mtu atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii anatenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Ufifilishaji makosa

13. Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kulipa kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi katika fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa TS Na. 34 la mwaka 2017

14. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2017 inafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

USHURU WA VITUO VYA KUOSHEA MAGARI

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kila kituo cha kuoshea Magari | 1,000/= kwa siku |

SEHEMU YA PILI
USHURU WA MACHINJIO

| Namba. | Aina ya Mifugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,500 kila mmoja |
| 2. | Mbuzi/ kondoo, Nguruwe | 1,500 kila mmoja |
| 3. | Kuku na aina nyingine ya ndege | 300 kila mmoja |

SEHEMU YA TATU
USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA

| Namba. | Aina ya Mifugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,500 kila mmoja |
| 2. | Mbuzi/kondoo, Nguruwe | 1,500 kila mmoja |
| 3. | Kuku na aina nyingine ya ndege | 200 kila mmoja |

SEHEMU YA NNE
USHURU WA MINADA YA MIFUGO

| Namba. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha ushurukwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe, Ngamia, Farasi, punda | 1,000 kwa kila aliyeuzwa |
| 2. | Mbuzi/ kondoo/nguruwe | 500 kwa kila aliyeuzwa |
| 3. | Vifaranga 100 wa siku moja (DOC) | 500 kwa kila boksi |
| 4. | Kuku na aina nyingine ya ndege | 300 kwa kila aliyeuzwa |

SEHEMU YA TANO

USHURU WA KUSAFIRISHA MIFUGO

| Namba. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kusafirisha mifugo nje ya eneo la Halmashauri | |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (a) | Ng'ombe | 2,500 kila mmoja |
| | (b) | Mbuzi/ kondoo, nguruwe | 1,500 kila mmoja |
| | (c) | Kuku, aina nyingine ya ndege | 500 kila mmoja |
| 2 | Ushuru wa kulaza mifugo inayosafirishwa eneo la Halmashauri | | |
| | (a) | Ng'ombe | 1,000 kila mmoja |
| | (b) | Mbuzi, kondoo na nguruwe | 500 kila mmoja |

SEHEMU YA SITA
USHURU WA NGOZI

| Namba. | Bidhaa | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ngozi ya ng'ombe | 500 kwa ngozi |
| 2. | Ngozi ya mbuzi/ kondoo | 200 kwa ngozi |
| 3 | Kibali cha usafirishaji wa ngozi kwa gari | 10,000 kwa ngozi za ng'ombe |
| | | 5,000 kwa ngozi za mbuzi |

SEHEMU YA SABA
USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| Namba | Aina ya Mazao | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya chakula | 3% ya bei ya soko |
| 2 | Mazao ya biashara | 3% ya bei ya soko |

SEHEMU YA NANE
USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Namba | Aina ya zao | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Mbao | 3% ya bei ya soko |
| 2 | Mkaa | 3% ya bei ya soko |
| 3 | Nguzo | 3% ya bei ya soko |
| 4 | Gogo | 3% ya bei ya soko |
| 5 | Mirunda | 3% ya bei ya soko |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Fito | 3% ya bei ya soko |
| 7 | Kuni | 3% ya bei ya soko |
| 8 | Veneer | 3% ya bei ya soko |
| 9 | Pallets | 3% ya bei ya soko |
| 10 | Asali na mazao yake | 3% ya bei ya soko |
| 11 | Mabanzi | 3% ya bei ya soko |
| 12 | Utomvu | 3% ya bei ya soko |

SEHEMU YA TISA
ADA YA LESENI ZA BIASHARA

| Namba. | Aina ya Leseni | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Leseni ya maduka ya dawa na vituo vya afya binafsi isipokuwa maduka na vituo vinavyomilikiwa na mashirika ya dini | 20% ya ada ya leseni |
| 2. | Leseni ya mazao ya misitu | 20% ya ada ya leseni |

SEHEMU YA KUMI
ADA YA KIBALI CHA UJENZI

| Namba. | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuweka mnara wa simu kwa kila mnara | 1,000,000 kwa mnara |
| 2. | Nyumba ya makazi | 300 mita ya mraba |
| 3. | Jengo la biashara | 500/= @ mita ya mraba |
| 4. | Kituo cha mafuta | 600/= @ mita ya mraba |
| 6. | Shule (binafsi) | 300/= @ mita ya mraba |
| 7. | Jengo la kutolea huduma za afya (binafsi) | 300/= @ mita ya mraba |
| 8. | Ghorofa makazi | 500/= @ mita ya mraba |
| 9 | Ghorofa biashara | 1000/= @ mita ya mraba |
| 9. | Ghala na bohari | 500/= @ mita ya mraba |
| 10. | Kiwanda | 600/= @ mita ya mraba |
| 11. | Majengo mengine | 300/= @ mita ya mraba |
| 12 | Makazi na biashara | 400/= @ mita ya mraba |
| 13 | Uzio wa mipaka jengo la makazi | 200/=@ mita ya mraba |
| 14 | Uzio wa mipaka jengo la biashara | 300/=@ mita ya mraba |
| 15 | Nyumba za ibada | 200/=@ mita ya mraba |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 16 | Viwanda vidogo | 300/=@ mita ya mraba |
| 17 | Parks, Garden, Play ground | 300/=@ mita ya mraba |
| 18 | Car wash | 300/=@ mita ya mraba |
| 19 | Fremu za biashara | 1,000/=@ mita ya mraba |
| 20 | Kuhuisha kibali | 50% ya ada ya kibali cha ujenzi wa jengo husika |
| 15 | Ukarabati | 50% ya ada ya kibali cha ujenzi wa jengo husika |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

ADA NA USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina ya madini | Kiwango cha ada na ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mawe | 1000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 2 | Kokoto | 2000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 3 | Tofali | 1500/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 4 | Mchanga | 1000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 5 | Kifusi | 1000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 6 | Udongo Mfinyanzi (Clay, Kaolin clay) | 10,000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 7 | Chokaa | 10,000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 8 | Marumaru | 10,000/= kwa kila tani moja ya uzito wa gari au chombo cha usafi. |
| 9 | Ada ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | 200@ mita ya mraba |
| 10 | Ada ya ukaguzi wa mazingira kwenye migodi ya madini ya Ujenzi | 500,000 kwa mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

ADA ZA USAJILI WA TEKSI, PIKIPIKI, BAJAJI NA GHARAMA ZA KUVUTA NA KUHIFADHI CHOMBO CHA USAFIRI

(i) Ada za usajili wa teksi, pikipiki, bajaji

| Namba. | Aina ya Chombo | Ada ya usajili kwa mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Teksi | 32,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Pikipiki | 10,000/= |
| 3. | Bajaji | 15,000/= |
| 4. | Pick-up | 20,000/= |
| 5. | Hiace | 20,000/= |
| 6. | Guta | 20,000/= |
| 7. | Lorry | 30,000/= |
| 8. | Double coster | 30,000/= |
| 9. | Canter | 25,000/= |
| 10 | Fuso | 30,000/= |

(ii). Gharama za kuvuta na kuhifadhi chombo cha usafiri

| Namba. | Aina ya Chombo | Gharama za kuvuta | Gharama za kuhifadhi kwa siku |
|---|---|---|---|
| 1. | Basi dogo la abiria chini ya 20 | 300,000/= | 50,000/= |
| 2. | Basi kubwa la abiria kati ya 20-28 | 300,000/= | 50,000/= |
| 3. | Basi kubwa la abiria zaid ya 28 | 300,000/= | 50,000/= |
| 4. | Teksi | 80,000/= | 50,000/= |
| 5. | Gari dogo binafsi | 80,000/= | 50,000/= |
| 6. | Lori na trela zaidi ya tani 3 | 300,000/= | 50,000/= |
| 7. | Lori na trela tani 3 na zaidi | 300,000/= | 50,000/= |
| 8. | Magari ya mizigo | 80,000/= | 50,000/= |
| 9. | Magari mengine | 300,000/= | 50,000/= |
| 10. | Pikipiki na bajaji | 50,000/= | 20,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TATU

ADA YA HUDUMA ZA KUMILIKI ARDHI

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kupitisha mchoro mpya | 300,000/= kwa mchoro |
| 2 | Kufanya marekebisho ya mchoro au kubadilisha matumizi | 200,000/= kwa mchoro |
| 3 | Fomu ya maombi ya viwanja | 20,000.00 @ kiwanja |
| 4 | Kupata barua ya toleo (drawing map) | 20,000.00@ kiwanja |
| 5 | Kuonyeshwa kiwanja kwa mara nyingine | 20,000.00@ kiwanja |
| 6 | Kufufua mipaka ya kiwanja | 30,000.00/=@ kiwanja |
| 7 | Utafiti binafsi wa taarifa za kiwanja (official search) | 40,000/=@ kiwanja |
| 8 | Kufanya uthamini kwa ajili ya kuhamisha umiliki | 80,000/=@ kiwanja cha Makazi |
| | | 100,000@ kiwanja Makazi na biashara |
| | | 500,000/=Viwanda/Taasisi |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

SEHEMU YA KUMI NA NNE
ADA YA MAOMBI YA ZABUNI

| Namba | Maelezo | | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya Maombi | | |
| | (a) | Kwa ngazi za msingi (vijiji na kata) | 20,000/= @zabuni |
| | (b) | Makao makuu ya Halmashauri zabuni ndogo | 50,000/=@ zabuni |
| | (c) | Zabuni ya kati | 100,000@ zabuni |
| | (d) | Zabuni kubwa | 150,000/=@ zabuni |
| 2 | Zabuni za vioski, vizimba, ofisi, mgahawa | | 10,000/=@ zabuni |

SEHEMU YA KUMI NA TANO
ADA YA KUWAPIMA WAHUDUMU

| Namba | Mhusika | Kiwango cha Ada (Shilihgi) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kuwapima afya wahudumu | 10,000/=@ mhudumu kwa miezi sita |

SEHEMU YA KUMI NA SITA
USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

| Namba | Aina ya Ushuru | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Nyumba za kulala wageni | Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atatozwa asilimia 10% ya mauzo ya vyumba vya kulala. |

SEHEMU YA KUMI NA SABA
ADA ZA UKODISHAJI WA MALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Maelezo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kumbi za Halmashauri | 200,000 kwa tukio kwa siku |
| 2 | Mashamba ya Halmashauri | 50,000/- kwa msimu wa kilimo wa zao husika. |
| 3 | Kifaa cha kupimia ardhi ”RTK” | 100,000/- kwa siku |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

SEHEMU YA KUMI NA NANE

ADA ZA UCHANGIAJI WA HUDUMA ZA USAFI

| Namba | Mchangiaji | Kiwango cha Ada kwa Mwaka (Shilingi) | Kiwango cha Ada Na Ushuru kwa Mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Taasisi za fedha/ mashirika/ kampuni (Microfinance, SACCOSS, Ofisi za Bima, mawakala wakubwa wa fedha,) | 150,000/= | 15,000/= |
| 2. | Benki | 300,000/= | 30,000/= |
| 3. | Taasisi za elimu/dini (kanisa /mskiti /day care) | 100,000/= | 10,000/= |
| 4. | Hospitali binafsi | 400,000/= | 40,000/= |
| 5. | Viwanda vikubwa | 600,000/= | 60,000/= |
| 6. | Viwanda vidogo | 300,000/= | 30,000/= |
| 7. | Karakana za Magari | 50,000/= | 5,000/= |
| 8. | Karakana za pikipiki/bajaji/baiskeli | 24,000/= | 2,000/= |
| 9. | Viwanda vya kuoka mikate | 300,000/= | 30,000/= |
| 10. | Hoteli kubwa | 300,000/= | 30,000/= |
| 11. | Baba lishe/mama lishe/vibanda vya chipsi | 36,000/= | 3,000/= |
| 12. | Useremala | 30,000/= | 4,000/= |
| 13. | Wauza mbao | 60,000/= | 6,000/= |
| 14. | Mashine ndogo za kusaga na kukoboa | 36,000/= | 3,000/= |
| 15. | Duka la jumla | 50,000/= | 5,000/= |
| 16. | Duka la rejareja | 36,000/= | 3,000/= |
| 17. | Ghala/godown. | 150,000/= | 30,000/= |
| 18. | Viwanda vidogo vya kukamua mafuta | 50,000/= | 5,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 19. | Bucha za samaki/nyama | 36,000/= | 3,000/= |
| 20. | Machinjio. | 300,000/= | 30,000/= |
| 21. | Mgahawa. | 60,000/= | 6,000/= |
| 22. | Baa | 100,000/= | 10,000/= |
| 23. | Mini super market. | 120,000/= | 15,000/= |
| 24. | Vilabu vya pombe za kienyeji kwa chumba kimoja. | 36,000/= | 3,000/= |
| 25. | Nyumba za kuishi kwa kaya | 12,000/= | 1,000/= |
| 26. | Saluni za ME na KE | 30,000/= | 2,500/= |
| 27. | Grocery | 30,000/= | 2,500/= |
| 28. | Nyumba za kulala wageni | 60,000/= | 6,000/= |
| 29. | Vituo vya afya na zahanati binafsi | 100,000/= | 10,000/= |
| 30. | Vituo vya mafuta | 150,000/= | 15,000/= |
| 31. | Duka la vifaa vya ujenzi (dogo) | 50,000/= | 5,000/= |
| 32. | Duka la Vifaa vya ujenzi (kubwa) | 100,000/= | 10,000/= |
| 33. | Maduka ya nguo na viatu | 60,000/= | 5,000/= |
| 34. | Maduka ya dawa [pharmacy] | 50,000/= | 5,000/= |
| 35. | Maduka ya dawa muhimu | 24,000/= | 2,000/= |
| 36. | Maduka ya mikate na vitafunwa | 12,000/= | 1,000/= |
| 37. | Maduka ya vyombo | 24,000/= | 2,000/= |
| 38. | Maduka ya kuuza magodoro na samani | 50,000/= | 5,000/= |
| 39. | Duka la vipodozi | 36,000/= | 3,000/= |
| 40. | Vibanda vya kuuza filamu/CD | 36,000/= | 3,000/= |
| 41. | Studio za picha/video | 36,000/= | 3,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 211 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 42. | Maduka ya jumla ya vinywaji moto na baridi | 50,000/= | 5,000/= |
| 43. | Fundi cherehani | 20,000/= | 2,000/= |
| 44. | Plastiki/chuma chakavu | 120,000/= | 10,000/= |
| 45. | Betting (bonanza/guru guru/pool table) | 36,000/= | 3,000/= |
| 46. | Casino/ Night club | 300,000/= | 30,000/= |
| 47. | Fundi kuchomelea/alminium | 50,000/= | 5,000/= |
| 48. | Vituo vya maziwa | 36,000/= | 3,000/= |
| 49. | Maua/miche ya miti/mapambo | 24,000/= | 2,000/= |
| 50. | Wachoma mahindi | 24,000/= | 2,000/= |
| 51. | Maabara za afya | 36,000/= | 3,000/= |
| 52. | Fundi sofa | 40,000/= | 4,000/= |
| 53. | Machinga | 24,000/= | 2,000/= |
| 54. | Maduka ya vioo | 50,000/= | 5,000/= |
| 55. | Vituo vya kuoshea magari | 36,000/= | 3,000/= |
| 56. | Duka la vipuri/ vilainishi | 36,000/= | 3,000/= |
| 57. | Matunda mboga mboga (nje ya soko) | 12,000/= | 1,000/= |
| 58. | Duka la pembejeo/mifugo | 36,000/= | 3,000/= |
| 59. | Mabanda ya mkaa/ kuni | 24,000/= | 2,000/= |
| 60. | Mabanda ya kuku | 24,000/= | 2,000/= |
| 61. | Stoo za matunda | 50,000/= | 5,000/= |
| 62. | Meza za sokoni | 24,000/= | 2,000/= |
| 63. | Kumbi za sherehe | 300,000/= | 30,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 64. | Huduma ndogo za kifedha | 36,000/= | 3,000/= |
| 65. | Stationery | 36,000/= | 3,000/= |
| 66. | Vifaa vya umeme | 36,000/= | 3,000/= |
| 67. | Gulio (kwa wiki) | | 1,000/= |
| 68. | Huduma ya choo/bafu | 50,000/= | 5,000/= |
| 69. | Wauza kahawa/ uji /tangawizi | 12,000/= | 1,000/= |
| 70. | Wauza miwa (Jumla) | 60,000/= | 5,000/= |
| 71. | Wauza miwa (reja reja) | 24,000/= | 2,000/= |
| 72. | Ushuru wa dampo kwa tripu 1 | 60,000/= | 5,000/= |
| 73. | Mtoa huduma za dawa za asili | 36,000/= | 3,000/= |
| 74. | Fundi TV/ Redio/ Simu/Kompyuta | 36,000/= | 3,000/= |
| 75. | Ofisi za kufua nguo (Dry cleaner/dobi) | 36,000/= | 3,000/= |
| 76. | Vituo vya mazoezi (GYM) | 36,000/= | 3,000/= |
| 77. | Fundi viatu | 12,000/= | 1,000/= |
| 78. | Ofisi za uchoraji wa ramani za majengo | 100,000/= | 10,000/= |

___________

JEDWALI LA PILI

______________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 13)*

FOMU YA KUFIFILISHA MAKOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Mji Mafinga, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Na kwamba niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo tarehe…………. ya mwezi…………..… mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU :
Jina:…………………………………..……………………......
Saini………………………….…………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Mafinga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Mafinga uliofanyika Tarehe 14 mwezi 02 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya ;-

AYOUB JUMA KAMBI
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji Mafinga*

REGNANT Z. KIVINGE
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji Mafinga*

NAKUBALI

/

**L.S**

Dodoma,
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*